



# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 (0)22-2122722/3  
 Nukushi: +255 (0)22-2130852  
 Barua pepe: dg@nbs.go.tz  
 Tovuti: www.nbs.go.tz

18 Barabara ya Kivukoni,  
 S.L.P. 796,  
 11992 - Dar es Salaam  
**TANZANIA.**



Unapojibu tafadhali taja:  
 Kumb Na: NBS/S.40/21/514

## YALIYOJITOKEZA

Tarehe: 08 Julai, 2016

### FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI JUNI 2016

### MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

#### **Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa**

Fahirisi za Bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Bei za bidhaa na huduma 278 zikiwa ni pamoja na bidhaa 97 za Vyakula na Vinywaji Baridi na 181 zisizo za Vyakula hukusanywa kila mwezi katika kila mkoa.

#### **Mizania Mpya za Bidhaa na Huduma na Jamii na Kizio cha Bei**

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijiji yaliyotokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2011/12. Kizio cha bei kinachotumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa ni cha mwezi Desemba, 2015.

#### **Makundi ya bidhaa na huduma za jamii**

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

#### **Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa**

Kuna maboresho mengi yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric mean of Price Relatives" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo; matumizi ya mfumo ulioboreshwu wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Mbinu na kanuni ya Lowe Index Formula ambayo ni aina ya "Laspeyres Index Formula" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZeka HADI ASILIMIA 5.5

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Juni, 2016 (Des., 2015 = 100)

Na. .	KUNDI (MAIN GROUP)	Mizania (Weight)	Juni-15	Mei-16	Juni-16	Badiliko la mwezi mmoja	Badiliko la miezi 12
1	Vyakula na vinywaji baridi	38.5	97.30	104.00	105.14	1.1	8.1
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.7	98.78	103.42	103.59	0.2	4.9
3	Mavazi ya nguo na viatu	8.3	97.95	101.91	102.43	0.5	4.6
4	Nishati, Maji na Makazi	11.6	99.61	108.33	107.14	-1.1	7.6
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.3	97.42	101.43	101.50	0.1	4.2
6	Gharama za Afya	2.9	97.10	102.98	103.75	0.7	6.8
7	Usafirishaji	12.5	98.02	98.83	99.25	0.4	1.3
8	Mawasiliano	5.6	99.59	98.89	99.04	0.2	-0.6
9	Utamaduni na Burudani	1.6	97.95	100.82	101.26	0.4	3.4
10	Elimu	1.5	99.68	102.37	102.37	0.0	2.7
11	Hoteli na Migahawa	4.2	98.54	103.44	103.77	0.3	5.3
12	Bidhaa na huduma nyinginezo	3.1	98.02	101.45	101.68	0.2	3.7
<b>JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE</b>		<b>100.00</b>	<b>98.10</b>	<b>103.00</b>	<b>103.47</b>	<b>0.5</b>	<b>5.5</b>
<b>Makundi Mengine Teule</b>							
1	Vyakula—vikijumuisha vyakula viliviyoliwa nyumbani na mahotelini Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula	37.07	97.57	104.54	105.66	1.1	8.3
2	Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta	8.68	99.77	108.07	107.22	-0.8	7.5
3		62.93	98.76	102.23	102.30	0.1	3.6
4		54.25	98.56	101.29	101.52	0.2	3.0

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Juni, 2016 umeongezeka hadi asilimia 5.5 kutoka asilimia 5.2 ilivyokuwa mwezi Mei, 2016. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Juni, 2016 imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2016. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 103.47 mwezi Juni, 2016 kutoka 98.10 mwezi Juni, 2015. Mfumuko wa Bei wa bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi mwezi Juni, 2016 umeongezeka hadi asilimia 8.1 kutoka asilimia 7.0 ilivyokuwa mwezi Mei, 2016.

#### **Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula**


Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwaka wa bidhaa za vyakula nyumbani na migahawani umeongezeka hadi asilimia 8.3 mwezi Juni, 2016 kutoka asilimia 7.2 mwezi Mei, 2016. Aidha, badiliko la Fahirisi za Bei kwa bidhaa zisizo za vyakula limepungua kidogo hadi asilimia 3.6 mwezi Juni, 2016 kutoka asilimia 3.8 mwezi Mei, 2016.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi Juni, 2016 umebaki kuwa asilimia 3.0 kama ilivyokuwa mwezi Mei, 2016.

Fahirisi inayotumika kukokotoa aina hii ya Mfumuko wa Bei, hajumuishi vyakula vinavyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa, kuni na umeme. Vyakula na bidhaa za nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara, hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

### Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Juni, 2015 hadi Juni, 2016. (Des., 2015 = 100)



Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, Fahirisi za Bei zimeonyesha mwenendo imara kutoka mwezi Juni, 2015 hadi mwezi Juni, 2016. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei nao umekuwa na mwenendo imara kutoka asilimia 6.1 mwezi Juni, 2015 hadi asilimia 5.5 mwezi Juni, 2016.

### MFUMUKO WA BEI WA MWEZI JUNI, 2016 KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZAKA KWA ASILIMIA 0.5

Mfumuko wa Bei wa mwezi Juni, 2016 unaopimwa kwa kipimo cha mwezi umeongezaka kwa asilimia 0.5, ongezeko sawa kama ilivyokuwa mwezi Mei, 2016. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 103.47 mwezi Juni, 2016 kutoka 103.00 mwezi Mei, 2016. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni pamoja na mahindi kwa asilimia 3.2, unga wa muhogo kwa asilimia 2.4, samaki wabichi kwa asilimia 3.8, maziwa mgando kwa asilimia 4.3, maharage mabichi yaliyomenywa kwa asilimia 6.1, kitunguu swaumu kwa asilimia 12.5, njegere kwa asilimia 6.2, viazi mviringo kwa asilimia 2.5, mihogo mibichi kwa asilimia 6.7, magimbi kwa asilimia 4.5, na ndizi za kupika kwa asilimia 2.7.

Kwa upande mwingine, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi za bei ni pamoja na huduma ya kinywa na meno kwa asilimia 13.8, mafuta ya dizeli kwa asilimia 2.4 na mafuta ya petroli kwa asilimia 4.3


## **THAMANI YA SHILINGI YA TANZANIA MWEZI JUNI, 2016 KUTOKA MWEZI DESEMBA, 2015**

Thamani ya Shilingi ya Tanzania hupima badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa Fahirisi za Bei za Taifa zinaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umefikia Shilingi 96 na senti 65 mwezi Juni, 2016 kutoka mwezi Desemba, 2015.

### **MIENENDO YA BEI**

#### **Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Mwezi Juni, 2015 hadi Juni, 2016. (Des, 2015 = 100)**



Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za Bei kuanzia mwezi Juni, 2015 hadi mwezi Juni, 2016. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi nyingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo jumuisha chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

#### **Jedwali Namba 2: Shajala ya Fahirsi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo**

Fahirisi za Bei za Taifa	Tarehe ya Toleo
Julai, 2016	08 <sup>th</sup> Agosti, 2016
Agosti, 2016	08 <sup>th</sup> Septemba, 2016
Septemba, 2016	08 <sup>th</sup> Octoba, 2016

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,  
Ofisi ya Taifa ya Takwimu**